# OFISI YA MAKAMU WA RAIS




NEWSLETTER MEI, 2019 TOLEO NAMBA 024



MHE. SAMIA SULUHU HASSAN
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



MHE. JANUARY Y. MAKAMBA
Waziri wa Nchi
(Muungano na Mazingira)



MHE. Mussa R. Sima
Naibu Waziri wa Nchi
(Muungano na Mazingira)



MHANDISI JOSEPH K.MALONGO
Katibu Mkuu



BALOZI JOSEPH E. SOKOINE
Naibu Katibu Mkuu



"Ndugu wananchi, mtakumbuka kwamba Serikali imepiga marufuku uingizaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 1 ya mwezi wa 6 mwaka huu wa 2019.

Marufuku hii haihusu vifungashio au plastiki zinazotumika ndani ya mifuko inayotumka kuhifadhia sukari, unga, saruji, mchele na bidhaa nyingne za aina hiyo.

Marufuku hii pia haitahusika kwenye plastiki zinazotumika kuhifadhia vimiminika kama maji, maziwa na mifuko inayotumika kwa shughuli za kilimo na mambo ya afya.

Ndugu zangu hii ni fursa pekee sasa kwa wafanyabiashara wadogo na wakubwa kuzalisha kwa wingi mifuko inayoruhusiwa kutumika ili kufanya Tanzania sasa kutumia mifuko inayofaa badala ya ile ya plastiki.

Ndugu zangu niwatake Watanzania wote kutokomeza mifuko ya plastiki kwa ustawi wa afya, mazingira na maendeleo ya nchi."

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN**
**MAKAMU WA RAIS WA TANZANIA**

# Waziri Makamba:Serikali haitaongeza muda marufuku ya mifuko ya plastiki

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. January Makamba amesema kuwa Ofisi yake kamwe haitarudi nyuma kusimamia katazo la matumizi ya mifuko ya Plastiki ifikapo Juni Mosi mwaka huu ingawa baadhi ya watu wamekuwa wakilalamika kuwa kipindi kilichotolewa ni kifupi.

Akizindua program maalumu ya kuelemisha umma juu ya "Marufuku ya Mifuko ya Plastiki nchini" Waziri Makamba amesema kuwa Kanuni zimeweka bayana aina ya mifuko ya plastiki iliyopigwa marufu na kuainishi aina za tozo na adhabu mbalimbali zitakazotolewa kwa kila kosa.

"Tumepiga marufuku uingizaji, usafirishaji, uhifadhi na matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini" hata hivyo kuna vifungashio ambavyo havitahusika na katazo hili mfano; vifungashio vya pembejeo za kilimo, madawa na baadhi ya vyakula," alisisitiza.

Alisema agizo hili limekuwa shirikishi na kusisitiza kuwa wadau wote muhimu walishirikishwa ikiwa ni pamoja na wenye viwanda na wazalishaji wa mifuko mbadala.

"Shirikisho la wenye viwanda waliniandikia barua na kuomba katazo la matumizi ya mifuko hii ya plastiki lianze kutumika mwezi Desema 2017, Serikali imetekeleza maombi haya mwaka mmoja baadae, sasa iweje watu walalamike kuwa muda hautoshi?" alihoji Waziri Makamba.

Waziri Makamba amewata wawekezaji kutumia fursa ya kuwekeza katika uzalishali wa mifuko mbadala na kusisitiza kuwa kuwa kupitia kikao na

Wazalishaji wa Mifuko mbadala wa plastiki kilichofanyika mapema mwezi huu wazalishaji wa mifuko mbadala wamethibitisha kuwa mbadala wa plastiki upo kwa kiasi cha kutosha.

Alisema wafanya biashara wenye mzigo/shehena kubwa ya mifuko ya plastiki wajitokeze ili Serikali iweke mazingira rafiki ya kuwezesha kuuza bidhaa hizo katika Nchi na mataifa mbalimbali ambako bidhaa hiyo itahitajika.

Aidha, Waziri Makamba ametoa onyo kwa 'viwanda bubu' ambavyo vimeendelea kuzalisha mifuko hiyo iliyopigwa marufuku na kusisitiza kuwa msako unaendelea.



Waziri Makamba (pichani) amesisitiza kuwa Serikali imeunda kikosi kazi kitakachoratibu utekelezaji wa zoezi hili kikosi kazi kinachojumuisha watendaji kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Mapato Tanzania na Idara ya Uhamiaji.

Taasisi zingine ni, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Shirika la Viwango Tanzania. Wengine ni Mamlaka ya Chakula na Dawa, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aprili 9 mwaka huu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alitangaza Juni Mosi 2019 kuwa mwisho wa matumizi ya Mifuko ya Plastiki hapa nchini.

# Serikali kuhakikisha mifuko mbadala inapatikana kwa wingi hapa nchini

Serikali imesema imejipanga kuhakisha kuwa mifuko mbadala wa plastiki inapatikana kwa wingi ili kukidhi mahitaji.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba katika Mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika Jijini Dodoma.

Alisisitiza kuwa katazo la Mifuko ya Plastiki lililotolewa jana na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa linakuwa na nguvu kisheria kwa kuandika kanuni za katazo ya mifuko ya plastiki zitakazotangazwa katika gazeti la Serikali chini ya Sheria ya Mazingira na kutoa adhabu kwa kila mtu atakaekiuka utaratibu uliowekwa. Mifuko mbadala

"Kabla ya Serikali kutangaza hatua ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki, ulifanyika utafiti na maandalizi ya mifuko mbadala. Uwezo wa kuzalisha upo na mifuko ya karatasi inayotumika Kenya na Rwanda inatumia malighafi inayozalishwa Mgololo-Iringa,Tanzania." Makamba alisistiza

Waziri Makamba ameainisha kuwa kuna vifungashio ambavyo havitapigwa marufuku ambavyo ni pamoja na vifungashio vya dawa za hospitalini, vifungashio katika sekta ya kilimo na ujenzi pia vile vya kuhifadhi maziwa na kutolea mfano wa vifungashio vya maziwa ya ASAS na Tanga Fresh, hata hivyo utaratibu maalumu utawekwa kwa wamiliki wa kukusanya vifungashio hivyo mara baada ya matumizi yake. Mif



*Mifuko mbadala*

Akizungumzia juu ya ushirikishwaji, Waziri Makamba amesema kuwa zoezi hili limekuwa ni shirikishi na hatua iliyotangazwa na Waziri Mkuu sio ya kushtukiza kwa kuwa Ofisi yake iliratibu mikutano katika maeneo kadhaa nchini kusikiliza maoni ya wananchi kuhusu zuio la mifuko ya plastiki.

Katika kukamilisha utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Waziri Makamba amesema Ofisi yake imeunda kikosi kazi cha kusimamia katazo hilo kikihusisha wajumbe kutoka

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Shirika la Viwango Tanzania.

Taasisi zingine ni Mamlaka ya Chakula na Dawa, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Wengine ni Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao cha Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri kilichofanyika katika ukumbi wa TAMISEMI jengo la Mkapa House jijini Dodoma.***




***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akihutubia wakati wa uzinduzi wa ripoti ya Mazingira Tanzania iliyoandaliwa na Benki ya Dunia pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira uliofanyika jijini Dar es Salaam.***



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. January Makamba akizungumza na wawakilishi kutoka kutoka taasisi mbalimbali wanaounda kikosi kazi cha kutekeleza agizo la kupiga marufuku mifuko ya plastiki nchini.***



***Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Balozi Joseph Sokoine akiongea na Waandishi wa habari jijini Dodoma wakati akitoa maelezo kuhusiana na zoezi zima la katazo la mifuko ya plastiki. Pembeni yakeni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira OMR Dkt Kanizio Manyika.***

# Wazalishaji Mifuko Mbadala wahakikisha soko la uhakika

Wazalishajji wa Mifuko Mbadala wamesema wamejipanga kukidhi mahitaji ya soko popote nchini na kwa muda muafaka wakati ambapo Serikali imepiga mifuko ya plastiki kuanzia Juni mosi mwaka huu.

Wamesema mifuko mbadala inayozingatia utunzaji wa mazingira ipo ya aina nyingi na wanatarajia kuwa itakuwepo ya kutosha kuendana na pia na ukuaji wa uchumi.

Wametoa kauli hiyo katika taarifa yao kwa umma ambapo wamesema tangu Serikali ilipotangaza katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki wazalishaji wa mifuko mbadala walianza kuona fursa na kuanza kuzalisha mifuko hiyo.

Waliongeza kuwa baada ya katazo hilo wazalishaji wa mifuko mbadala wameongeza kasi ya uzalishaji na tayari wameagiza mashine kwa ajili ya kuanza uzalishaji huo.

Aidha, walibainisha kuwa wazalishaji wa mifuko mbadala wameanza kutoa mafunzo kwa watu mbalimbali na tunawaomba watanzania kuona fursa ya mifuko hiyo ikiwa ni sehemu ya kujitengenezea kipato.

"Tunawahakikishia wananchi na wadau mbalimbali wanaotaka kuwekeza kwenye fursa hii kuwa malighafi inapatikana sehemu mbalimbali nchini kwa mfano karatasi inapatikana Mufindi Paper Mills Ltd na Tanpack Tissues Ltd.

"Malighafi ya vitambaa laini inapatikana Harsho Group mjini Moshi, mikeka, katani na pamba vinapatikana maeneo mbalimbali nchini pia vitambaa vya nguo vinapatikana madukani na soko kuu la Kariakoo," walisisitiza.

Walitoa mwito kwa Watanzania kuona fursa ya mifuko mbadala kuwa ni sehemu ya kujitengenezea kipato kwani wazalishaji wameanza kutoa mafunzo kwa watu mbalimbali.

Walishauri Serikali na taasisi husika kutoa mafunzo na teknolojia ya kutengeza mifuko mbadala na kuwa halmashauri zielekeze misaada na mikopo kwa vikundi au watu wanaoingia kwenye uchumi huu mpya wa mifuko hiyo.

Walizishauri Serikali za Mikoa na Halmashauri mbalimbali kuelekeza nguvu zao kukuza uchumi wa wananchi wao kwa kuwekeza kwenye mifuko mbadala na kwa kufanya hivyo itasaidia kuondoa upungufu utakaojitokeza sambamba na kuchochea uchumi na kuacha mazingira salama.

Katazo la mifuko ya plastiki lilitangazwa Aprili 10, 2019 lilitangazwa bungeni na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa na linasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ikishirikiana na kikosi kazi kutoka taasisi mbalimbali.



# Yafahamu madhara mbalimbali ya kutumia mifuko ya plastiki

Hivi karibuni Serikali ilipiga marufuku uzalishaji, uingizaji, usafirishaji nje ya nchi, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko aina ya plastiki maarufu kama 'rambo' inayotumika kubebea bidhaa.

Katazo hilo lililotangazwa bungeni jijini Dodoma Aprili 9, 2019 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa tayari limeanza kutekelezwa na ifikapo Juni mosi, 2019 ni mwisho wa matumizi yote ya mifuko hiyo.

Katika kusimamia katazo hilo na kuhakikisha linatekelezwa kwa ufanisi, Ofisi ya Makamu wa Rais yenye dhamana ya kusimamia utunzaji wa Mazingira imeunda kikosi kazi ambacho kinaundwa na taasisi mbalimbali za Serikali.

Serikali imechukua hatua madhubuti za kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo ili kuepusha athari mbalimbali za kiafya zinazoendelea kujitokeza.

Inawezekana wananchi wengi wamekuwa na mazoea ya kutumia mifuko ya plastiki kubebea bidhaa mbalimbali hususan za vyakula bila kujali athari za mifuko hiyo kwa afya za binadamu, wanyama na mazingira.

Mifuko hii baada ya matumizi imekuwa ikitupwa ovyo na hata ikitupwa kwenye mashimo ya taka huweza kupeperushwa kwa upepo na kusambaa hivyo husababisha uchafuzi wa mazingira. Hata ikichomwa moshi wake una athari kwa binadamu.

Pia mifuko ya plastiki haiwezi kuoza kwa haraka katika mazingira wanadamu walipo kwani inakadiriwa kuweza kudumu hadi zaidi ya miaka 500 na hivyo kuleta athari za muda mrefu n ahata ikichomwa huleta madhara ya kiafya.

Huweza kusababisha saratani kwa binadamu kwani inapotumika kuhifadhia chakula cha moto, joto la chakula husika linachanganyika na plastiki hiyo na kutengeneza kemikali ambazo ni sumu.

Mifuko ya plastiki inapochomwa huweza kusababisha uchafuzi wa hewa ambayo ikivutwa na binadamu husababisha saratani na kuathiri mfumo wa upumuaji.

Madhara mengine yanayoweza kutokea ni kusababisha mafuriko katika maeneo ambayo kuna mifereji kutokana na kuziba kwa miundombinu ya majitaka na mifereji ya mvua.

Kama ambavyo binadamu wanavyoweza kupata athari kutokana na matumizi ya mifuko hiyo hususan katika kubebea vyakula, pia wanyama nao huweza kuathirika.

Wanyama mbalimbali ikiwemo mifugo kama ng'ombe, mbuzi au kondoo wanaweza kufa wanapoila na kuimeza mifuko hii.



*Inaendelea Uk. 7*

# Madhara ya mifuko ya plastiki

*Inatoka Uk. 6*

Katazo hili linatolewa kauli na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. January Makamba ambaye anasema Serikali itahakikisha linakuwa na nguvu kisheria.

Anasema Serikali imeandaa kanuni za katazo hilo na tayari zimetangazwa katika gazeti la Serikali chini ya Sheria ya Mazingira na kutoa adhabu ya faini au kifungo kwa mtu atakayekiuka utaratibu uliowekwa.

Akizungumzia juu ya ushirikishwaji, Waziri Makamba anabainisha kuwa katazo hilo la mifuko ya karatasi limekuwa ni shirikishi na hatua iliyotangazwa na Waziri Mkuu si ya kushtukiza.



*Waziri wa Nchi OMR, Mhe. January Makamba alipokutana na wadau wa mifuko ya plastiki*

Anasema kuwa Ofisi yake tayari ilisharatibu mikutano katika maeneo kadhaa nchini na kusikiliza maoni ya wananchi kuhusu katazo hilo la mifuko ya plastiki.

Waziri Makamba anasisitiza kuwa Serikali itasimamia kikamilifu katazo hilo ifikapo tarehe hiyo ingawa baadhi ya watu wamekuwa wakilalamika kipindi kilichotolewa ni kifupi.Itakumbukwa kuwa awali Serikali ilitangaza kuzuia matumizi yote ya mifuko ya plastiki kuanzia Januari mosi, 2017.

Hata hivyo baada ya mashauriano na Shirikikisho la la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) na umma ilikubali kusogeza mbele hadi Desemba 31, 2017 ili kutoa muda kwa wajasiriamali, umma na CTI kujiandaa na utekelezaji wa katazo hilo.

Kwa kutambua umuhimu na ukubwa wa jambo hilo, Serikali haikuanza kulitekeleza Januari mosi, 2018 ili kutoa muda wa ziada kwa wadau hao kujipanga zaidi. Hivyo kutokana na hilo katazo lilisogezwa mbele hadi kufikia Juni mosi, 2019 kama ambavyo imetangazwa na kutoa muda wa kutosha wa matayarisho

Serikali imeunda kikosi kazi kitakachoratibu utekelezaji wa zoezi hilo ambacho kinajumuisha watendaji kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Mapato Tanzania na Idara ya Uhamiaji.

Taasisi zingine ni Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Hata hivyo hivyo, Waziri Makamba anawaondoa hofu wananchi kwa kusema kuwa katazo hilo la mifuko ya plastiki halitahusu baadhi ya vifungashio vya bidhaa zikiwemo maziwa, mikate, pembejeo za kilimo, ujenzi, dawa na baadhi ya vyakula kama korosho na vinywaji kama maziwa ambavyo ni ni lazima vikidhi viwango vilivyowekwa na TBS).

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA




*Naibu Waziri wa Nchi OMR-Muungano na Mazingira, Mhe. Mussa Sima (kulia) akizungumza katika kipindi cha 'Tujadiliane' kinachoandaliwa na wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na kurushwa na vyombo mbalimbali vya habari nchini. Kushoto ni mwendesha kipindi, Dotto Bulendu.*




*Naibu Waziri wa Nchi OMR-Muungano na Mazingira, Mhe. Mussa Sima (wa pili kulia) akioneshwa na kukabidhiwa mfuko mbadala na Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Abubakar Karsan.*



*Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Kati Mwalimu Carlos Mbuta (kulia) akmsikiliza mfanyabiashara katika soko la majengo jijini Dodoma ambaye bado anatumia mifuko ya plastiki ambaye aliahidi kuiacha kabla ya Juni 1. Tukio hilo lilifanyika wakati kikosi kazi kilichofanya opeesheni maalumu kufuatilia namna katazo la kifuko ya plastiki linavyotekelezwa katika maeneo mbalimbali jijini humo.*



Afisa wa mazingira katika jiji la Dodoma, Ali Mfinanga (aliyeshika mfuko) ambaye ni sehemu ya Kikosi kazi cha marufuku ya mifuko ya plastiki akizungumza na mfanyabiashara katika soko la majengo jijini Dodoma wakati kikosi kazi hicho kilichofanya ziara kuangalia namna katazo la mifuko ya plastiki linavyotekelezwa.


ISHU YA MIFUKO YA PLASTIKI KAMA SIJAIELEWA VIZURI VILEEE!
USIUMIZE KICHWA BRO, NAMBI HIZO HAPO, WAPIGIE HAUTACHAJIWA
KUPIGA BILA MALIPO
0800 110 115, 0800 110 116, 0800 110 117, 0800 110 118, 0800 110 119
SMS/WHATSAPP
+255 737 796 253, +255 737 796 252, +255 737 796 251
+255 737 796 250, +255 737 796 249


STOO NINA MIFUKO YA PLASTIKI FIBAO!!!
KIOSKI
SHAKA ONDOA, WATATANGAZA VITUO VYA KUKUSANYIA


UMEPIGA STOP MIFUKO YA PLASTIKI, TUTABEBEA NINI?!
KUNA MIFUKO YA GUNIA, NGUO NA VIKAPU..
... BILA KUSAHAU VIWANDA VYA MIFUKO MBADALA ZAIDI YA 75, VYA KARATASI VIKIWEMO
SERIKALI

## Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Ofisi ya Makamu wa Rais


## MAWASILIANO:


**S.L.P. 2502**<br>
**Dodoma, Tanzania**<br>
**Simu: +255 266 235 2038**<br>
**Fax: +266 235 0002**<br>
**Barua pepe: ps@vpo.go.tz**<br>
**km@vpo.go.tz**<br>
**Tovuti: www.vpo.go.tz**<br>
**Facebook: Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania**<br>
**Whatsapp: 0685 333 444**